

# MAOMBI NI HALISI... TUOMBE

Pastor James Kalekwa

# Maombi ni halisi... TUOMBE!

James Kalekwa

## Orodha ya Yaliyomo

Tabaruku ....................................................................... 4

Salamu na Utangulizi ........................................................ 5

SURA YA KWANZA: UNATAFUTWA! ........... 7

SURA YA PILI: UHALISIA WA UWEPO WA ULIMWENGU WA ROHO ................................................10

Nalikuwa katika roho ....................................................10

Ngazi ya Yakobo “Beth-el” ............................................11

Maombi ndiyo njia pekee ya mawasiliano baina ya ulimwengu wa roho na wa mwili. ....................................13

SURA YA TATU: MGUSO WA MAOMBI YANGU .........17

SURA YA NNE: NAMNA YA KUOMBA ...23

MFALME: ........................................................................24

Kuhani ...........................................................................25

Kuomba Kama Mfalme: .................................................25

Ulimwengu wa roho wa Matamko (Declaration and Decrees) ........................................................................31

KUHANI: .........................................................................33

Kuhusu Mwandishi: ..........................................................43

Kuhusu New Vine Church: ................................................43

Mawasiliano na Mwandishi: ...............................................44

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

# Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma

yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# SURA YA KWANZA: UNATAFUTWA!

Kupitia somo hili, nimekusudia kukusaidia kujibu swali la kwa nini watu hawaombi; kwa nini watu hawaombi kuhusu agenda fulani-fulani; na kwanini watu hawajihusishi kwenye maombi kwa nguvu… Yote yanajibiwa na swala la ufahamu kuhusu uhalisia (The realities) wa swala zima la maombi.

Kwenye ulimwengu wa ukristo, maombi ni moja ya mada inayofundishwa sana kuliko kutendwa… kujifunza kuhusu kuomba, na kuomba ni vitu viwili tofauti. Kujifunza kuhusu kufunga, na kufunga ni vitu viwili tofauti. Mtu mmoja mwenye hekima alisema, namna bora ya kujifunza kuogelea, ni kuogelea! Nimekuja kufika kwenye hitimisho hili, namna bora ya kujifunza kuomba, ni kuomba.

*“[30] Nami nikatafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma, na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu, lakini sikuona mtu. [31] Kwa sababu hiyo*

*nimemwaga ghadhabu yangu juu yao; nimewateketeza kwa moto wa hasira yangu; nami nimeileta njia yao wenyewe juu ya vichwa vyao, asema Bwana MUNGU.”* Ezekieli 22:30-31

i. Mungu anatafuta mtu – mmoja; na si watu wengi! Kwa Mungu, aina hii ya mtu, mwombaji, ni sawa na nchi nzima. Mtu anayeweza kuwahifadhi wengine kwa njia ya maombi.

ii. Ajabu na kweli mtu wa namna hii anaweza kukosekana kwenye nchi… kuna wananchi LAKINI **mtu** (mwombaji) anaweza kukosekana. Kwa somo hili, Mungu asikose mtu Tanzania.

iii. Nchi alimwagiwa ghadhabu ya Mungu si kwa sababu ya uwingi wa dhambi zao au kiwango cha uovu uliokuwa unaendelea wakati huo, bali ni kwa sababu ya kukosekana mwombaji mmoja tu!

iv. Kwa kuongeza, anaweza akawepo mwombaji mmoja lakini asiombe kama anavyotarajiwa, madhara yake ni makubwa… uwepo wa mwombaji asiyeomba, ni sawa na kutokuwepo kabisa – Unakumbuka kisa cha Sodoma na Gomora? Miji ilichomwa kwa sababu Ibrahimu hakuomba mpaka mwisho wa ombi Rejea: Mwanzo 18:16-33

*"Akasema, Bwana asiwe na hasira, nami nitasema mara hii tu, Huenda wakaonekana huko kumi? Akasema, Sitaharibu kwa ajili ya hao kumi."* Mwanzo 18:3

Hakuna ukomo au zuio la kimaombi ambalo Ibrahimu aliwekewa. Angweza kusema kwamba Mungu akikuta mwenye haki mmoja?

Kwa kuwa hakuomba mpaka mwisho, pia majibu ya maombi yake yalikuja ila kwa kupishana sana. Ni kweli Mungu aliwahifadhi wenye haki lakini nje ya Sodoma na Gomora. Angeweza kuwahifadhia ndani kitu ambacho kingemaanisha kuhifadhiwa kwa miji hiyo.

# SURA YA PILI: UHALISIA WA UWEPO WA ULIMWENGU WA ROHO

Ulimwengu wa roho si jambo la kufikirika. Ni jambo halisia na kweli. Watu wengi hawaombi kwa kiwango kinachotarajiwa kwa sababu ya upungufu wa uelewa kuhusu uhalisia wa ulimwengu wa roho. Kuna vitu wakijua tu, wataanza kuomba.

## Nalikuwa katika roho

*"Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo,* ***nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo****, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.* ***Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana****; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu,"* Ufunuo wa Yohana 1:9-10

**Nalikuwa katika kisiwa cha Patmo** – eneo la kimwili. Anwani inayofikika kimwili (physical address). Patmo ni kisiwa kilichopo "Asia ndogo" kweye nchi ya Uturuki ya sasa.

**Nalikuwa katika roho** – Ni jambo la kuvutia kugundua ya kwamba Yohana, mtume alikuwa sehemu nyingine tena wakati huo huo. Ukisoma kwa umakini, kitabu chote cha ufunuo ni maelezo ya kinachoendelea *"katika roho"* wakati huo na wakati ujao miaka mingi *"Apocalyptic"*. Kwa hiyo, mwanadamu anaweza kuwa sehemu mbili kwa wakati mmoja… katika mwili "Patmo" na katika roho!

**Ngazi ya Yakobo "Beth-el"** Ref: Mwanzo 28:12 –18 *"Mungu yuko hapa na mimi sikujua!"* Ninapenda sana huo mshangao. Wengi hawajui kuhusu uwepo wa Mungu (wanajua kwa maarifa ya kichwa na si kwa mioyo na maisha yao na kwa kuhusiana). Hawana utambuzi wa ulimwengu wa roho na uhaisia wake.

Huo mshangao ni kuonyesha ya kwamba laity kama angejua mahali hapo ni "Beth-el": *Beth* ni nyumba na *El* ni Mungu. Kama angefahamu mahali pale ni nyumba ya Mungu angefanya nini unafiriki? Angeishia kuchukua jiwe na kulaza kicha tu? La hasha! Si unaona baada ya kugundua alichana na shughuli za kulala… aliachana na mambo ya mwili akaanza kufanya ibada.

*"Yakobo akaondoka asubuhi na mapema, akalitwaa lile jiwe alililoliweka chini ya kichwa chake,* ***akalisimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake****. 19Akaita jina la mahali pale* ***Betheli****; lakini jina la mji ule hapo kwanza uliitwa Luzu.* ***20Yakobo akaweka nadhiri akisema****, Mungu akiwa pamoja nami, akinilinda katika njia niiendeayo, na kunipa chakula nile, na nguo nivae; 21nami nikirudi kwa amani nyumbani kwa baba yangu, ndipo BWANA atakuwa Mungu wangu.* ***22Na jiwe hili nililolisimamisha kama nguzo litakuwa nyumba ya Mungu****; na katika kila utakalonipa* ***hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi.****"* Mwanzo 28:18-22

Unaona matukio ya kiroho yaliyofuatia baada ya ugunduzi ule. Kuna uelewa ukiwa nao, huwezi kusinzia. Huwa ninawaambia vijana kuna usingizi halafu kuna usingizi… kuna usingizi ambao ni matokeo ya ujinga hali ya kutokujua.

Unaposoma sura hii, ninaomba kutambulisha kwako kweli hii ya kwamba hapo ulipo na namna unavyohusiana na ulimwengu wa roho kwenye maombi ni udhihirisho wa ufahamu wako. Kuna mengi ya kujua. Ninakuombea kwa

Bwana ya kwamba atakushangaza… atajifunua kwako na kukupa Beth-el *experience* yako!

## Maombi ndiyo njia pekee ya mawasiliano baina ya ulimwengu wa roho na wa mwili.

*"Mwatamani, wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala* ***hamna kitu kwa kuwa hamwombi****! Hata mwaomba, wala* ***hampati kwa sababu mwaomba vibaya****, ili mvitumie kwa tamaa zenu."* Yakobo 4:2-3

Mzee Yakobo anaonyesha kwanini watu hawana vitu wanavyopenda au kutamani... kwa sababu hawaombi au wanaomba vibaya. Vitu usivyokuwa navyo katika uhalisia, ni ushahidi wa vitu usivyoviombea/viomba. Matokeo unayoyatamani lakini huyashiki mkononi ni maeneo ambayo unaomba vibaya.

Mt 7:7-8 SUV *"**Ombeni, nanyi mtapewa**; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; **kwa maana kila aombaye hupokea**; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa."*

Yesu amefundisha kwa kurudia mara nyingi sana kuhusiana na uhalisia wa maombi. Kiasi cha kukufanya ugundue Mungu hutenda duniani kwa kuyaitikia maombi ya watakatifu (God works on earth in response to the prayers of the saints). Kama kuna mwanadamu wa kuomba, kuna Mungu wa kujibu!

Mathayo 6:5, "Tena msalipo msiwe kama wanafiki..."

Mathayo 6:7, "Nanyi mkiwa katika kusali..."

Mathayo 6:9, "Basi ninyi salini hivi..."

Mathayo 6:16, "Tena mfungapo..."

Yohana15:16, "Si ninyi... ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu wapeni."

Ukifuatilia historia ya kanisa la mwanzo (Matendo ya Mitume) kisha karne ya kwanza ya kanisa, utagundua ya kuwa maombi yalikuwa ndiyo mwitikio wa asili wa

waamini (prayer was a natural response of belivers). Waliyaamini maombi bila kusaza (without reservations). Walikuwa naive kiasi hicho... waliyaamini maombi *literally*! Hawakusema maombi kwa kiebrania yanamaanisha nini… hawakuchambua maombi kwa kiyunani yana mizizi mingapi ya neno… hawakuchimba muktadha wa maombi. Waliomba!

Unakumbuka kisa cha Petro gerezani? Kwenye Matendo ya Mitume 12 ni tukio linahusisha kiongozi wa kiserikali/kisiasa/mamlaka dhidi ya waamini... ungetarajia waitikieje? Wao waliomba!

Ungetarajia watafute namba za liwali mmoja.. ungetarajia wazungumze wa kiongozi wa maakida… ungefikiri itakuwa nyepesi zaidi kutoa tamko, kulaani vitendo viovu, kuandamana, kushinikiza serikali ya Herode. Ingekuwa ni sawa zaidi kwa kuwa wanashughulika na mwanasiasa na hii vita hata *"siyo ya kiroho"* ni mambo ya kisiasa.

Kimantiki kama inakuja hivi… lakini si kweli na si sawa! Kinyume chake, WALIOMBA!

Yakobo 5:13-14, *“Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? **Na aombe**... mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; **nao wamwombee**...”*

Utakuja kugundua kuomba ndiyo mila na desturi ya kambi hii. Kuna ufahamu ukiwa nao, basi utatenda kama kanisa la mwanzo.

# SURA YA TATU: MGUSO WA MAOMBI YANGU

Kwenye sura hii nimekusudia kukuonyesha maombi yanaweza kutokeza matokeo gani na matokeo kiasi gani. Ninataka hatimaye ujisemee moyoni… TUOMBE!

Nitatumia mfano wa mtu mmoja aliyeomba na kugeuza uelekeo wa kalenda ya nchi na ulimwengu kimajira.

**“Nabii” Danieli**

Wasifu wa mwombaji huyu ni mrefu lakini ngoja tuutazame kwa kifupi. Kusudio langu ni kukupa changamoto ya kwamba hakuwa mtu asiye na jambo la kufanya kwa hiyo akaamua kuomba.

Dan 2:49 SUV *“[49] Tena, Danieli akamwomba mfalme, naye akawaweka Shadraka, na Meshaki, na Abednego, wawe juu ya mambo yote ya uliwali wa Babeli; lakini huyo* ***Danieli alikuwa akiketi katika lango la mfalme****.”*

Alisimama na awamu tatu mfululizo za kiutawala: Nebukadreza, Evil-Merodaki (2 Fal 25:27-30/Yer. 52:31-34) Belishaza, Dario na Koreshi.

Huyu ni mtu aliyezoea kutembea kwenye korido za mamlaka. Anajua maswala ya itifaki na utawala.

Tunaambiwa kuhusu wasifu wake wa kimaombi:

Danieli 6:10 – *Mara tatu kwa siku*

Danieli 10:13 – *Siku ishirini na moja*

Danieli 2:17-18 – *Ad hoc basis (Hitaji lilipokuja);* vs. 11 "miungu wasiofanya kikao na wanadamu..."

Sasa, ukisoma kwenye Danieli 10:11-14, 20 (Mfalme wa Uajemi) vs. Mstari wa kwanza – Danieli anaushughulisha ulimwengu wake wa roho na siyo wa mwili. Unaona kuna mtu na kuna roho wote wanatambulishwa kama "Mfalme/Mkuu/Mtawala wa Uajemi."

Mtawala wa kwanza wa Uajemi ni huyu Mfalme anayeitwa Koreshi.

*"Katika mwaka wa tatu wa* ***Koreshi, mfalme wa Uajemi****, Danieli, ambaye jina lake aliitwa Belteshaza, alifunuliwa*

*neno; na neno lile lilikuwa kweli; maana ni vita vikubwa; naye akalifahamu neno lile, akaelewa na maono hayo"* Danieli 10:1

Halafu kuna huyu mwingine ambaye ni kiumbe kisicho cha kimwili – kiumbe roho naye anatambulika kama mkuu wa Uajemi.

*"Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja; bali, tazama, huyo Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wa mbele, akaja kunisaidia; nami nikamwacha huko pamoja na wafalme wa Uajemi. 14Sasa nimekuja kukufahamisha mambo."* Danieli 10:13-14

Danieli yuko kwenye maombi ya kutaka uhuru kwa ajili ya watu wake wa Yuda kutoka uhamishoni warudi kwao. Biblia inatuambia alisoma vitabu, akagundua ya kwamba kwa kalenda za kinabii walipaswa kuwa huru.

*"katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, mimi Danieli,* ***kwa kuvisoma vitabu, nalifahamu hesabu ya miaka, ambayo neno la BWANA lilimjia Yeremia nabii,***

***ya kuutimiza ukiwa wa Yerusalemu, yaani, miaka sabini.****”* Danieli 9:2

Tunajua kwa njia ya Maandiko Mtakatifu ya kwamba kutokea hapo, Danieli aliamua kuomba na si kufanya tukio lolote lile.

*“**Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu**, ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga, na kuvaa nguo za magunia na majivu.”* Danieli 9:3

Unaona, kujua kulimpelekea kuomba! Huwa ninapenda sana kusema hili, kujua kwingi kutaonekana kwa kuomba kwingi. Ukijua halafu usiombe basi hujui… au nikikuhurumia nitasema unajua vibaya.

Turudi kwenye wafalme wa Uajemi… Wakati maombi yanaendelea pale nyumbani kwake, kumbe kuna vurugu zinaendelea katika ulimwengu wa roho. Kuna viumbe wanatishiana uhai… wanatunishiana misuli na wanaonyeshana ubabe.

Ni jambo gani limefungulia vurugu zote hizo. Ni maombi ya mtu mmoja mzuri wa Mungu. Ili ujue hakuwa anajifurahisha tu au kupoteza muda wake, ninataka uone

ni kwa namna gani maombi yake yalianza kutokeza katika ulimwengu wa mwili.

Ezr 1:1 SUV *“[1] Ikawa katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, ili kwamba neno la BWANA alilolisema kwa kinywa cha Yeremia lipate kutimizwa,* ***BWANA akamwamsha roho yake Koreshi, mfalme wa Uajemi, hata akapiga mbiu katika ufalme wake wote, akaiandika pia, akisema****,”*

Nani alimsha roho ya Koreshi, mfalme wa uajemi? Ni Bwana! Ndiyo ni Bwana… alifanya hivyo kama jibu kwa maombi ya Danieli.

Angalia Bwana anavyoyaitikia maombi:

Isa 44:28 SUV *“[28]* ***nimwambiaye Koreshi, Mchungaji wangu,*** *naye atayatenda mapenzi yangu; hata ataunena Yerusalemu, Utajengwa; na hilo hekalu, Msingi wako utawekwa.”*

*“Haya ndiyo* ***BWANA amwambiayo Koreshi, masihi wake,*** *ambaye nimemshika mkono wake wa kuume, ili kutiisha mataifa mbele yake, nami nitalegeza viuno vya*

*wafalme; ili kufungua milango mbele yake, hata malango hayatafungwa." Is. 45:1*

Koreshi anarejelewa na Mungu kama masihi na mchungaji… mtu ambaye Bwana anamtumia kukamilisha makusudi yake mwenyewe.

Koreshi, mfalme wa Uajemi asema hivi;

*"BWANA, Mungu wa mbinguni, amenipa falme zote za dunia;* ***naye ameniagiza nimjengee nyumba katika Yerusalemu, ulioko Yuda****."* Ezra 1:2

*"Lakini katika mwaka wa kwanza wa* ***Koreshi, mfalme wa Babeli, Koreshi, mfalme, alitoa amri ijengwe tena nyumba ya Mungu.****"* Ezra 5:13

Unaona jinsi Danieli anauchezea moyo wa mfalme kutokea kwenye chumba cha maombi? Mfalme anajikuta anaongea vitu ambavyo hata yeye hakuwa ampangilia sana kuviombea. Maombi yameumua moyo wake!

Kalenda ya dunia ilihama – taifa la Israeli likarudi kutoka uhamishoni kwa maombi ya mtu mmoja, na kujenga

hekalu lililobomolewa la Sulemani: Zerubabeli, Ezra na Nehemia ndiyo waliongoza awamu za kurejea kutoka uhamishoni.

# SURA YA NNE:
# NAMNA YA KUOMBA

Unaweza kumweleza mtu nini cha kufanya, kwa nini afanye, lini afanye… LAKINI usipompa namna ya kufanya utakuwa umemdhulumu pakubwa sana. Watu wengi wamejaa hamasa wasiyojua ni kwa namna gani waitekeleze.

Ni kweli tumefundishwa mengi kuhusu maombi. Nimeona vyema kwa njia ya kitabu hiki kuwasilisha kwako namna gani tunafaa tuombe hususani tunapozungumzia uombezi (intercession).

Ufunuo 5:9-10 *"Nao waimba mpya wakisema, wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa,*

*ukawafanya kuwa* ***wafalme na makuhani*** *kwa Mungu wetu: nao wanamiliki juu ya nchi"*

Wafalme na Makuhani ni nafasi za watiwa mafuta (the anointed ones). Ni vyema ufahamu ya kwamba mtiwa mafuta hupokea mafuta kwa ajili ya kazi maalum. Mteule wa raisi na muapishwa wa raisi – siyo kwa ajili ya kujisikia vizuri bali ni kwa ajili ya kazi.

**MFALME:**

- ✓ Husimama kwa ajili na kwa niaba ya Mungu mbele za watu
- ✓ Ni mtu anayetunga sheria
- ✓ Ni mtu anayesimamia utendaji na utekelezaji wa sheria

Note: Wafalme walipokuwa wakiend kinyume na sheria ya Bwana, kuna kundi jipya likainuka – MANABII. Check and Balance ya mamlaka ya kifalme

**Kuhani**: ni mtu ambaye yuko kwa niaba ya Mungu kwa wanadamu;

- ✓ Husimama kwa ajili na kwa niaba ya watu mbele za Mungu.
- ✓ Mwanadamu anayezungumza na Mungu kwa niaba ya wanadamu wenzake; akipeleka mahitaji ya wanadamu wenzake mbele za Mungu. Kuhani anafanya hivyo kwa ridhaa na bila ridhaa ya watu.

## Kuomba Kama Mfalme:

Ni vyema ufahamu ya kwamba kuna lugha za wafalme, watawala na wenye mamlaka. Na wao wanapoisikia huwa wanaelewana.

Mfano:

Mt 8:8-9 SUV *“[8] Yule akida akamjibu, akasema, Bwana, mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu;* ***lakini sema neno tu****, na mtumishi wangu atapona. [9] Kwa maana* ***mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia***

***huyu, Nenda, huenda; na huyu, Njoo, huja; na mtumwa wangu, Fanya hivi, hufanya.****"*

Mwitikio wa Yesu kwenye lugha hii ya mamlaka:

*"[9] Yesu aliposikia hayo alimstaajabia, akaugeukia mkutano uliokuwa ukimfuata, akasema,* ***Nawaambia, hata katika Israeli sijaona imani kubwa namna hii****. [10] Na wale waliotumwa waliporudi nyumbani,* ***wakamkuta yule mtumwa ni mzima.****"* Lk. 7:9-10

Yesu alielewa na kukubaliana na lugha hii ya mamlaka na kuitafsiri kuwa ni imani.

Namna ya kumwomba Mungu kutokea kwenye nafasi ya ufalme :

1) Kusimika amri

1 Fal 17:1 SUV *"[1] Basi Eliya Mtishbi, wa wageni wa Gileadi, akamwambia Ahabu, Kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele zake,* ***hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii, ila kwa neno langu****."*

Biblia inatuonyesha ya kwamba kulikuwa na mambo ambayo yangefanyika kwenye nchi, Mungu angeifunga mvua. Mojawapo ya hayo mambo ni kuiabudu miungu mingine… kuabudu sana mu na miungu ya kigeni kama vile ni Mungu wa kweli.

Sasa, Nabii Eliya alikuwa analifahamu neno la Mungu na utendaji wake. Alilichukua na kuliweka kwenye kinywa chake kwa niaba ya Mungu. Moyo wake unawaka kwa hasira ambayo Mungu mwenyewe angewaka kuhusiana na ibada ya miungu namna ile katika ya watu wake.

Kum 11:16-17 SUV, *"[16] Jitunzeni nafsi zenu, mioyo yenu isije ikadanganywa, mkageuka na kutumikia miungu mingine na kuiabudu; [17] hasira za BWANA zikawaka juu yenu, naye akafunga mbingu kusiwe na mvua, wala nchi isitoe matunda yake; mkaangamia kwa upesi mtoke katika nchi nzuri awapayo BWANA."*

Zek 14:17 SUV,*"Tena itakuwa, ya kwamba mtu awaye yote wa jamaa zote zilizomo duniani, asiyekwea kwenda Yerusalemu ili kumwabudu Mfalme, BWANA wa majeshi, mvuahaitanyeshakwao."*

Kwa hiyo aliposema mvua haitanyesha kwa neno langu… haikuwa majivuno bali ilikuwa ni lugha ya unyenyekevu wa kiwango cha juu sana! Hilo ndilo jukumu la mwombaji kama mfalme.

1 Fal 16:31-33 SUV, *"[31] Ikawa, kama ingalikuwa neno dogo tu kuyaendea makosa ya Yeroboamu mwana wa Nebati, akamwoa Yezebeli binti Ethbaali, mfalme wa Wasidoni, akaenda akamtumikia Baali, akamsujudia. [32] Akamjengea Baali madhabahu katika nyumba ya Baali, aliyoijenga huko Samaria. [33] Ahabu akaifanya Ashera; Ahabu akazidi kumghadhibisha BWANA, Mungu wa Israeli, kuliko wafalme wote wa Israeli waliomtangulia."*

2) Kutoa hukumu & haki

Rejea maandiko ya hapo juu. Mojawapo ya jambo alilokuwa akilifanya Eliya kama mwombaji ni kutoa hukumu na haki kwa yale ayaliyokuwa yakiendelea juu ya nchi. Alifanya hivyo kwa ajili na kwa niaba ya Mungu.

3) Maagizo (Matangazo, Amri na Matamko)

Dan 4:16-17 SUV *“[16] moyo wake ubadilike, usiwe moyo wa binadamu, na apewe moyo wa mnyama; nyakati saba zikapite juu yake. [17]* ***Hukumu hii imekuja kwa agizo la walinzi, na amri hii kwa neno la watakatifu; kusudi walio hai wapate kujua ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu****, naye humpa amtakaye, tena humtawaza juu yake aliye mnyonge.”*

Hii ni “Press Release” ya Mfalme Nebukadreza baada ya akili kumrejea [Miaka 7 akiwa ni mnyama kabisa]. Anatoa maelezo juu ya hali ya afya ya akili yake. Anaonyesha kuna mahali fulani kuna waombaji ndiyo kimsingi wanaoongoza maswala ya ikulu. Kisha anaelezea sababu ya hayo yote: *“…kusudi walio hai wapate kujua ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu…”*

Lengo la haya yote si kujisifu au kutafuta utukufu binafsi bali ni kumjulisha Mungu kwa watu.

4) Kusudio (Nia au msimamo wa ndani)

*"[28] **Nawe utakusudia neno**, nalo litathibitika kwako; Na mwanga utaziangazia njia zako. [29] Hapo watakapokuangusha, **utasema,** Kuna kuinuka tena; Naye mnyenyekevu Mungu atamwokoa."* Ayu. 22:28-29

Maombi ya ufalme hutaka watu wenye msimamo wa ndani kuhusu mambo fulani. Kisha wanaoweza kuyatamka makusudio waliyonayo. Biblia inatuelekeza ya kwamba wakati hali iko jinsi fulani, "Utasema" Na kile utakachokisema kitakuwa kinyume na jinsi hali ilivyo, unalewa mfalme?

Umewahi kumsikia moja ya wanamatengenezo wa kanisa wa kale kule nchini Uskochi (Scotland) John Knox (1513–1572). Alifahamika kwa ombi lake moja mashukuri: "Give me Scotland, Lord, or I die!" ndivyo alivyomwomba Mungu! (Mungu nipe nchi Uskochi la sivyo nife tu)

Malkia wa Uskochi amenukuliwa akimuongelea mtumishi huyu kwa kusema:

*“I fear the prayers of John Knox more than all the assembled armies of Europe.”*

(Ninayaogopa maombi ya John Knowx kuliko majeshi yote ya viya ya Ulaya yakikusanyika pamoja) Malkia Mary, Mtawala wa Scotland

Fikiria mtu anaomba na kuipeleka mbio nchi na mamlaka namna hiyo!

Kwenye kaburi la Know pameandikwa maneno yafuatayo: “Here lies one who never feared any flesh.” (Hapa amaelala yule aliyekuwa hatishwi na yeyote mwenye mwili).

## Ulimwengu wa roho na Matamko (Declaration and Decrees)

Hapo juu nimetambulisha ya kwamba kuomba katika roho kunahusisha kufanya matamko (declarations and decrees). Ninapenda tujadili jambo hilo hapa kwa kutumia migfano ya Biblia. Nitakusihi ujishikilie na usome kila andiko nililolinukuu kwa sababu haliko kwa bahati mbaya.

1. Watunzi wa mashauri mabaya juu ya mji/nchi Ref: Ezekieli 11:1-4 *"1.Tena roho ikaniinua, ikanileta hata lango la upande wa mashariki wa nyumba ya BWANA, lililoelekea upande wa mashariki; na tazama, mahali pa kuingilia pa lango walikuwako watu ishirini na watano; na katikati yao nikamwona* ***Yaazania, mwana wa Azuri, na Pelatia, mwana wa Benaya, nao ni wakuu wa watu.*** *2. Akaniambia, Mwanadamu,* ***hawa ndio watu wale watungao uovu, na kutoa mashauri mabaya ndani ya mji huu; 3. wasemao, Wakati wa kujenga nyumba si karibu; mji huu ni sufuria na sisi ni nyama.*** *4.* ***Basi toa unabii juu yao, Ee mwanadamu, toa unabii.*** *5. Roho ya BWANA ikaniangukia, naye akaniambia, Nena, BWANA asema hivi; Mmesema maneno hayo, Enyi nyumba ya Israeli; maana mimi nayajua yaingiayo katika mioyo yenu."*

Unaona suluhisho alilopewa nabii dhidi ya watu wanaotunga mambo mabaya kwa watu na ujenzi wa nyumba ya Bwana… Anaambiwa awatolee unabii:

Kutoa unabii:

- Kusema (speak forth) – kufungua kinywa na kutamka.
- Kuyasema mapenzi ya Mungu (kweli ya Mungu) kuhusiana na jambo fulani.
- Kusema kuhusu mambo yajayo na mambo ya siri na mafumbo.

Unaweza kufungua kinywa chako na kutamka? Fanya hivyo sasa kama mfalme!

**KUHANI:**

Nitatumia rejea nyingi ya maandiko katika kuitambulisha dhana hii. Ambatana na mimi ili ufuate mtiririko wa wazo.

i. Asili ya Ukuhani na Utendajikazi wake:

Ni vyema ukajua ya kwamba ukuhani kwa Mungu Yehova, ulianza baada ya Utumwa wa Misri (Post-Egypt Slavery Era). Ukuhani ulianza na Haruni kisha ukaenda kwa wanawe – ukawa ni utumishi wa familia.

Mungu anautaja ukuhani kuwa ni kazi maalum "katika kazi". Ninapenda ujue, ukuhani (na hasa kwa uelewa wa

shule ya maombi), siyo jukumu la watu wasio na kazi. Bali ukuhani ndiyo kazi yenyewe.

Kuhani alikuwa ni "Mtakatifu kwa Bwana" – Mtu aliyetengwa kwa ajili ya matumizi maalum (kuwekwa wakfu).

Kut 28:1,12,29,30,36 SUV

"[1] Nawe umlete Haruni ndugu yako karibu nami, na wanawe pamoja naye, miongoni mwa wana wa Israeli, ili ***anitumikie katika kazi ya ukuhani***. Haruni, na Nadabu, na Abihu, na Eleazari, na Ithamari, wana wa Haruni.

[12] Nawe utavitia vile vito viwili juu ya vipande vya mabegani vya hiyo naivera, viwe vito vya ukumbusho kwa ajili ya wana wa Israeli; ***naye Haruni atayachukua majina yao mbele za BWANA juu ya mabega yake mawili ili kuwa ukumbusho.***

[29] ***Na Haruni atayachukua majina ya wana wa Israeli katika kile kifuko cha kifuani cha hukumu juu ya moyo wake, hapo atakapoingia ndani ya mahali patakatifu***, kuwa ukumbusho mbele ya BWANA daima. [30] Nawe utie hizo Urimu na Thumimu katika kile kifuko cha

kifuani cha hukumu; ***nazo zitakuwa juu ya moyo wa Haruni,*** hapo atakapoingia ndani mbele ya BWANA; na ***Haruni atachukua hukumu ya hao wana wa Israeli juu ya moyo wake mbele ya BWANA daima.***

[36] Nawe fanya bamba la dhahabu safi na kuchora juu yake, mfano wa machoro ya muhuri, **MTAKATIFU KWA BWANA.**”

Umeona jukumu la kuhani kuanzia kwenye namna vazi lake lilivyokuwa likiandaliwa? Ninafikia hitimisho ya kwamba kuhani hayupo kwa ajili yake mwenyewe badala yake yuko kwa ajili ya watu wengine. Anawachukua watu… anachukua hukumu zao… anachukua majina yao… Huo uzito wote uko kwenye mabega ya kuhani!

Hii siyo mitaa ya kuomba mkate wetu wa kila siku, mpendwa!

ii. Mfano wa Danieli

Dan 9:3-5 SUV, *“[3] Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga, na kuvaa nguo za magunia na majivu. [4] Nikamwomba BWANA, Mungu wangu, nikaungama, nikasema, Ee Bwana, Mungu mkuu, mwenye kutisha, ashikaye maagano na rehema kwao wampendao, na kuzishika amri zake; [5] tumefanya dhambi, tumefanya ukaidi, tumetenda maovu, tumeasi, naam, hata kwa kuyaacha maagizo yako na hukumu zako;”*

Soma kwa kulinganisha na:

Yer 25:1-13 SUV, “[1] Neno hili ndilo lililomjia Yeremia, katika habari za watu wote wa Yuda; katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu, mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda mwaka ule ndio mwaka wa kwanza wa Nebukadreza, mfalme wa Babeli; [2] ambalo Yeremia, nabii, aliwaambia watu wote wa Yuda, na wenyeji wote wa Yerusalemu, kusema, [3] Tangu mwaka wa kumi na tatu wa kutawala kwake Yosia, mwana wa Amoni, mfalme wa Yuda, hata siku hii ya leo, miaka hii ishirini

na mitatu, neno la BWANA limenijia, nami nimesema nanyi, nikiamka mapema na kusema; lakini ninyi hamkusikiliza. [4] Naye BWANA ametuma kwenu watumishi wake wote, hao manabii, akiamka mapema na kuwatuma, lakini ninyi hamkusikiliza, wala hamkutega masikio yenu, msikilize. [5] Akasema, Rudini sasa, kila mtu na aiache njia yake mbaya; uacheni uovu wa matendo yenu, mkae katika nchi ambayo BWANA aliwapa, ninyi na baba zenu, tangu zamani za kale na hata milele; [6] wala msiwafuate miungu mingine, ili kuwatumikia na kuwasujudia, wala msinikasirishe kwa kazi ya mikono yenu; basi, mimi sitawadhuru ninyi kwa dhara lo lote. [7] Lakini ninyi hamkunisikiliza, asema BWANA; ili mnikasirishe kwa kazi ya mikono yenu, na kujidhuru nafsi zenu. [8] Basi BWANA wa majeshi asema hivi, Kwa kuwa hamkuyasikiliza maneno yangu, [9] angalieni, nitapeleka watu na kuzitwaa jamaa zote za upande wa kaskazini, asema BWANA, nami nitatuma ujumbe kwa Nebukadreza, mfalme wa Babeli, mtumishi wangu, nami nitawaleta juu ya nchi hii, na juu yao wakaao ndani yake, na juu ya mataifa haya yote yaliyopo pande zote; nami nitawaangamiza kabisa, na kuwafanya

kitu cha kushangaza, na kitu cha kuzomewa, na ukiwa wa daima. [10] Tena, nitawaondolea sauti ya kicheko, na sauti ya furaha, sauti ya bwana arusi, na sauti ya bibi arusi, sauti ya mawe ya kusagia, na nuru ya mishumaa. [11] Na nchi hii yote pia itakuwa ukiwa, na kitu cha kushangaza; nayo mataifa haya watamtumikia mfalme wa Babeli miaka sabini. [12] Na itakuwa miaka hiyo sabini itakapotimia, nitamwadhibu mfalme wa Babeli, na taifa lile, asema BWANA, kwa sababu ya uovu wao, nayo nchi ya Wakaldayo pia; nami nitaifanya kuwa ukiwa wa milele. [13] Nami nitaleta juu ya nchi ile maneno yangu yote niliyoyanena juu yake, naam, yote yaliyoandikwa ndani ya kitabu hiki, aliyotabiri Yeremia juu ya mataifa haya yote."

Pata muda wa kulinganisha na maandiko haya pia:

Yer 29:10-14 SUV, "[10] Maana BWANA asema hivi, Babeli utakapotimiziwa miaka sabini, nitawajilia ninyi, na kulitimiza neno langu jema kwenu, kwa kuwarudisha mahali hapa. [11] Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu

za mwisho. [12] Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza. [13] Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote. [14] Nami nitaonekana kwenu, asema BWANA, nami nitawarudisha watu wenu waliofungwa, nami nitawakusanya ninyi, nikiwatoa katika mataifa yote, na katika mahali pote, nilikowafukuza, asema BWANA; nami nitawaleta tena, hata mahali ambapo kutoka hapo naliwafanya mchukuliwe mateka."

Dan 9:2-3 SUV, "[2] katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, mimi Danieli, kwa kuvisoma vitabu, nalifahamu hesabu ya miaka, ambayo neno la BWANA lilimjia Yeremia nabii, ya kuutimiza ukiwa wa Yerusalemu, yaani, miaka sabini. [3] Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga, na kuvaa nguo za magunia na majivu."

Unaona jinsi Danieli anaomba kama kuhani?

iii. Mfano wa Nehemia:

"[2] Hanani, mmoja wa ndugu zangu, akanijia, yeye na watu wengine waliotoka Yuda; nami nikawauliza habari za Wayahudi waliopona, hao watu wa uhamisho waliosalia; na habari za Yerusalemu. [3] Wakaniambia, Watu wa uhamisho, waliosalia huko katika wilaya ile, wamo katika hali ya dhiki nyingi na mashutumu; tena ukuta wa Yerusalemu umebomolewa, na malango yake yameteketezwa kwa moto. [4] *Hata ikawa niliposikia maneno hayo, nikaketi, nikalia, nikaomboleza siku kadha wa kadha; kisha nikafunga, nikaomba mbele za Mungu wa mbinguni; [5] nikasema, Nakusihi, Ee BWANA, Mungu wa mbinguni, Mungu mkuu, mwenye kuogofya, mwenye kutimiza agano lake na rehema zake kwa hao wampendao na kuzishika amri zake; [6] tega sikio lako, macho yako yakafumbuke, upate kuyasikiliza maombi ya mtumishi wako, ninayoomba mbele zako wakati huu, mchana na usiku, kwa ajili ya wana wa Israeli, watumishi wako; hapo ninapoziungama dhambi za wana wa Israeli, tulizozifanya juu yako; naam, mimi na nyumba ya baba yangu tumefanya dhambi.*" Neh. 1:2-6

iv. Mfano wa Anna binti Fanueli:

“[25] Na tazama, pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni, naye ni mtu mwenye haki, mcha Mungu, akiitarajia faraja ya Israeli; na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. [26] Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristo wa Bwana. [27] Basi akaja hekaluni ameongozwa na Roho; na wale wazazi walipomleta mtoto Yesu ndani, ili wamfanyie kama ilivyokuwa desturi ya sheria, [28] yeye mwenyewe alimpokea mikononi mwake, akamshukuru Mungu, akisema, [29] Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, Kwa amani, kama ulivyosema; [30] Kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako,

[36] Palikuwa na nabii mke, jina lake Ana, binti Fanueli, wa kabila ya Asheri, na umri wake ulikuwa miaka mingi, alikuwa amekaa na mume miaka saba baada ya uanawali wake. [37] Naye ni mjane wa miaka themanini na minne; haondoki katika hekalu, ila huabudu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba. [38] Huyu alitokea saa ile ile akamshukuru Mungu, na wote waliokuwa wakiutarajia

ukombozi katika Yerusalemu akawatolea habari zake." Lk. 2:25-30, 36-38

Kwa ujumla wake:

Utagundua kwa ushahidi mwingi wa maandiko na mifano iliyoambatanishwa ya kuwa maombi ya kikuhani hujumuisha mambo yafuatayo.

I. Toba
   - ✓ Mwombaji anajihusisha moja kwa moja na kosa
   - ✓ Utambuzi wa kosa/dhambi bila kutoa visingizio
   - ✓ Utambuzi ya kwamba stahiki ya dhambi ni adhabu

II. Ufahamu wa Agano/Ahadi ya Mungu

III. Utambuzi wa mamlaka huru ya Mungu (Sovereignty) – akitaka kusamehe anaweza; akitaka kuadhibu anaweza!

IV. Utambuzi wa uweza (siyo uwezo) wa Mungu – Utegemezi kwa Mungu

V. Hali ya kupondeka moyo na kunyenyekea

VI. Moyo wa shukurani

Kama maombi ni jambo halisi hivi, si tuinuke tuombe sasa?

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi  wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.


Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**





New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11)*.

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

## Ratiba za Ibada

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa
+255 754 917 764
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
MchungajiJK
+255 754 917 764